CITIZENS 4 CHANGE

# Maendeleo ya Awali ya Mtoto

Kulia ni njia ya mtoto wako ya kuwasiliana na kuhusiana na wewe.

## Kweli nne kuhusu watoto wanaolia:

### Kweli #1

Pale mtoto mchanga anapolia na kuacha baada ya wewe kumbembeleza kwa utulivu, ni ishara ya uhusiano mzuri kati yako na mwanao.

### Kweli #2

Mtoto mchanga anayelia anaweza kuwa anataka kukuambia kuwa;

- Anahisi njaa
- Amechoka
- Amechukia
- Anataka kucheza

### Kweli #3

Mtoto mchanga anayelia sana au ambaye halii kabisa anaweza kuwa na msongo wa mawazo. Kilio chake kinaweza kuwa ni ishara ya uhusiano mbaya baina yake na mlezi.

### Kweli #4

Hisia za watoto wachanga zinahusiana sana na zile za walezi wao. Unapokuwa na msongo wa mawazo mtoto wako hulia mara kwa mara na unapokuwa mtulivu, mtoto hufarijika.